# HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI MKUBWA WA HALMASHAURI TAREHE 31 /10/2021

**MAHUDHURIO**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndugu. Maria .P. Leshalu | Mwenyekiti |
| 2. | Ndugu. Evod .F. Cgang'ambwe | Katibu |
| 3. | Ndugu Godfrey Ayako | Mjumbe |
| 4. | Ndugu. Noel .K. Abel | Mjumbe |
| 5. | Dr. Rahim Hangai | Mjumbe |
| 6. | Eng. Cyprian Warioba | Mkaribishwa |
| 7. | Ndugu. Mwajuma .S. Mlacha | Sekretarieti |

**Muht Na 07/2021 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 08:20 Mchana

**Muht Na 08/2021 KUTHIBITISHA AGENDA**

Jumla ya agenda 6 ziliwasilishwa na kupokelewa na wajumbe kama ifuatavyo;

1. Kufungua kikao
2. Kupokea na kuthibititisha
3. Taarifa ya tathimini ya zabuni ya uchimbaji wa visima katika vijiji vya Ngh'ambi, Mbugani, Kiegea na shule ya msingi Idilo.
4. Mpendekezo ya bodi ya Zabuni ya uchimbaji wa visima katika vijiji vya Ngh'ambi, Mbugani, Kiegea na shule ya msingi Idilo.
5. Kuidhinisha matumizi ya Force Account katika ujenzi wa miradi ya majosho, vituo vya afya vya Mbori na Ipera na ujenzi wa madarasa 83 katika shule za sekondari na madarasa 20 katika shule za msingi( Shule sikizi)
6. Kufunga kikao

**Muht Na 09/2021 TAARIFA YA TATHIMINI YA UCHIMBAJI WA VISIMA KATIKA VIJIJI VYA NGH'AMBI, MBUGANI, KIEGEA NA SHULE YA MSINGI IDILO**

Kuliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilipokea fedha kiasi cha Tsh 235,000,000/= kwa ajili ya uchimbaji wa visima vitatu katika vijiji vya Mbugani, Ngh'ambi na Kiegea. Mchakato wa kumpata Mzabuni ulianzia kwa kutoa nukuu za bei kwa Wazabuni kuanzia tarehe 16/08/2021 kwa kuchukua vitabu ambapo wazabuni watatu ndio waliochukua vitabu vya zabuni:

1. Nangwai Enlighted Drillers Co LTD
2. Make Engineering and Water Works LTD
3. Zionane Contractors and Genersl Supplier Co. LTD

Zabuni zilifunguliwa tarehe 30/08/2021 katika ukumbi wa Halmashauri kwa Wazabuni wote watatu kuhudhuria. Ufunguzi wa zabuni na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:

1. Kwa upande wa visima vitatu vya Ngh'ambi na Kiegea

a. Nangwai Engineering Drillers Company Limited. Gharama aliyoiweka ni Tsh 120,448,503.00
b. Make Engineering and Water Works Limited. Gharama aliyoiweka ni Tsh 107,509,800.00
c. Zionanane Contractors and General Suppliers Co LTD. Gharama aliyoiweka ni Tsh 124,324,800.

2. Kwa upande wa kisima kimoja cha shule Msingi Idilo matokeo yalikuwa kama ifuatavyo;
   a. Nangwai Engineering Drillers Company Limited. Gharama aliyoiweka ni Tsh 101,568,500.00
   b. Make Engineering and Water Works Limited. Gharama aliyoiweka ni Tsh 59,318,600.00
   c. Zionanane Contractors and General Suppliers Co LTD. Gharama aliyoiweka ni Tsh 67,525,000/=

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri aliwateua wajumbe wanne wa kamati ya tathimini ya zabuni ya uchimbaji wa visima ambaoni;

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Joseph Malangalila | (Mhasibu) | Mwenyekiti |
| 2. | Nuru Simkoko | (Mhandisi) | Katibu |
| 3. | Jackson Marco | (Mhandisi) | Mjumbe |
| 4. | Charles Ngwembele | (Tekinishiani) | Mjumbe |

Kamati ilitoa matokeo kwa wazabuni wote ikionesha vigezo vya kila Mzabuni na kisha kuwasilishwa kwenye Bodi ya zabuni.

**Muht Na 10/2021 MPENDEKEZO YA BODI YA ZABUNI YA UCHIMBAJI WA VISIMA KATIKA VIJIJI VYA NGH'AMBI, MBUGANI, KIEGEA NA SHULE YA MSINGI IDILO**

Kuliwasilishwa taarifa kutoka kwa Kamati ya Tathimini ya Zabuni ya uchimbaji wa visima ambapo wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipitia taarifa kurasa moja moja na kisha kumpendekeza Mzabuni Make Engineering and Water Works Limited kuwa ndiye Mzabuni aliyekidhi vigezo vyote vinavyohitajika na kuwa mwenye gharama ndogo ya uchimbaji kwa Tsh 107,509,800 Hivyo basi apewe mkataba wa uchimbaji wa visima vitatu vya vijiji vya Ngha'mbi, Mbugani na Kiegea na kisima kimoja cha shule ya Msingi Idilo. Baada ya mapendekezo hayo Bodi ilipendekeza Mhandisi Cyprian Warioba Meneja kutoka RUWASA kutoa ufafanuzi kuhusu namna kazi hizo zitakavyofanyika, ambapo alishauri kuwa zoezi la kuanza kuchimba visima ni vyema likaanza haraka kwani zoezi linaweza kukwama endapo msimu wa mvua utaanza. Ushauri mwingine ulioutowa ni juu ya mradi wa uchimbaji kisima shule la msingi Idilo ambapo Mhandisi alishauri kuwa kwa kuwa fedha ya mradi ipo shuleni taarifa ya Mzabuni aliyeshindwa zabuni ipelekwe shuleni kwa ajili ya uwamuzi zaidi. **Wajumbe walipokea ushauri ulitolewa na kisha kushauri yafuatayo;**

1. **Katika mradi wa uchimbaji wa kisima Idilo makubaliano yafanyike kati ya mwajiri na Mzabuni aliyeshinda zabuni kutokana na bajeti ya mradi kuwa ndogo ukilinganishwa na kiasi ambacho Mzabuni amekionesha kwenye mchanganuo wake mradi.**

2. **Bodi imeshauri barua ziandikwe kwa Wazabuni ambao wameshindwa na yule aliyeshinda naye apatiwe barua. Hii ni kwa miradi ya Ngh'ambi, Mbugani na Kiegea.**
3. **Kabla ya kusaini mkataba Menejimenti ihakikishe nyaraka zote muhimu za Mzabuni ziwe zimethibitishwa na Mwanasheria.**
4. **Performance of Bond na Bank guarantee ziwepo endapo Mzabuni ataomba malipo ya awali.**
5. **Kibali cha uchimbaji (Permit drilling) kiwepo**
6. **Force Account itumike katika mradi wa kisima shule ya Msingi Idilo. Hii ni kutokana na kuwepo kwa utofauti wa fedha baina ya kiasi cha fedha kilichowasilishwa na Mzabuni na kiasi cha fedha kilichopo kwenye akaunti ya shule.**

**Muht Na 10/2021 KUIDHINISHA MATUMIZI YA FORCE ACCOUNT KATIKA UJENZI WA MAJOSHO NA UJENZI WA MADARASA YA UVICO 19**

Kuliwasilishwa taarifa kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) imetenga jumla ya Tsh 3,033,441,000 kwa ajili ya ujenzi wa majosho 169 katika Halmashauri 70 nchi nzima. Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa imepatiwa jumla ya 36,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa majosho mawili ya Pwaga na Godegode. Kulitolewa maelezo kuwa ili kuweza kukamilisha ujenzi wa majosho yenye viwango vinavyohitajika kwa kutumia utaratibu wa Force Account.

**Wajumbe walipokea taarifa iliyowasilishwa kuwa kuna fedha za miradi ya ujenzi madarasa kwa Idara ya Elimu msingi ambapo imetengewa jumla ya Tsh 400,000,000 na Idara ya Elimu Sekondari imetengewa jumla ya Tsh 1,660,000,000 kisha kupitisha kuwa miradi ya ujenzi huo itumie Force Account.**

**Muht Na 11/ 2021 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 10: 45 Jioni

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ........................ | ........................ |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**TAREHE** 21/12/2021